Taarifa kutoka City of Burlington kuhusu COVID-19

Burlington COVID-19 Resource and Recovery Center (RRC)

Machi 2021

(Kiswahili)

Vidokezo:

- *Aina mpya ya virusi imepatikana Vermont*
- *Taarifa ya kusafiri ya jimbo*
- *Tangazo la jimbo kuhusu mikusanyiko*
- *Chanjo za bila malpo sasa zinapatikana kwa watu walio na miaka 65 na zaidi*
- *Chanjo kwa watu walio na hali za afya za hatari ya juu iliyokadiriwa Machi baadaye*
- *Jinsi ya kujisajili kwa ajili ya chanjo*
- *Mpango wa usaidizi wa upangaji wa dharura*

Aina Mpya ya Virusi

Mpango wa City's Wastewater Monitoring ***umepata aina tofauti ya COVID-19 huko Burlington ambayo mara ya kwanza ilipatikana Uingereza****. Taarifa hii si chanzo cha kuzua wasiwasi, lakini ni tahadhari kwa jamii kutumia hadhari ya ziada. Inakadiriwa kuwa* ***aina hizi mpya za virusi zinaweza kusambaa asilimia 30 hadi 40 haraka zaidi*** *kuliko uzao wa COVID-19 ambao kwa sasa uko katika jamii.* ***Tafadhali saidia kudhibiti msambao kwa kufanya yafuatayo:***

Endelea kuepuka mkusanyiko na familia nyingine na kufuata mwongozo wa Jimbo

Vaa barakoa zisizo na chini ya matabaka mawili zenye ubora wa juu ambazo zimeunganishwa vizuri ili kupunguza mapengo

Kupimwa COVID-19 ikiwa una dalili yoyote, umesafiri, au umehudhuria mkusanyiko wa kijamii.

Kupata chanjo ya COVID-19 ikiwa unastahiki

Taarifa ya Kusafiri ya Jimbo

Mwongozo wa kusafiri wa Vermont umesasishwa. ***Watu waliopata chanjo kikamilifu na wamekaa nje siku 14 kutoka kwenye chanjo yao ya mwisho wanaweza kusafiri kuelekea na kutoka Vermont bila vikwazo vya karantini.*** *Mbali na hayo, mtu aliyepata chanjo kikamilifu anayetangamana na mtu aliyethibitishwa kuwa na COVID-19 hatahitajika kuenda karantini.* ***Yeyote ambaye HAJAPATA chanjo kikamilifu lazima aingie karantini inayohitajika wakati wa kurudi au kusafiri kuelekea Vermont****. Wakazi wa Vermont wanaorudi kutoka ziara ya nje ya jimbo lazima wakamilishe karantini ya siku 14 au karantini ya siku 7 ikifuatiwa na kipimo kisicho na virusi.*

Tangazo la Jimbo kuhusu Mikusanyiko

Mikusanyiko ya kijamii *inayohusisha familia nyingi, ndani na nje ya nyumba, katika maeneo ya umma na faragha* ***HAIRUHUSIWI kwa watu ambao hawajapata chanjo****wakati huu.* ***Watu au familia zilizopata chanjo zinaweza kukutana tu na familia nyingine moja iliyopata chanjo au isiyopata chanjo moja baada ya nyingine.*** *Biashara na mashirika bado haviruhusiwi kufanya mikutano ya familia nyingi iwe wahudhuriaji wamechanjwa au bado.*

Ili kuona mwongozo wa Jimbo kwa Kiingereza, tembelea:
https://accd.vermont.gov/news/update-new-work-safe-additions-be-smart-stay-safe-order

Usambazaji wa Chanjo

Chanjo salama na zinazofanya kazi za COVID-19 sasa zinapatikana kwa watu walio Vermont ambao wana miaka 65! Wanaokuja bila miadi wanakubaliwa kwa sasa na watu lazima waweke miadi mapema. Bima haihitajiki na chanjo ni ya BILA MALIPO.

Chanjo zinapatikana kwa sasa kwa:

- *Watu wa Vermont wa umri wa miaka 65 na zaidi*
- *Wafanyakazi wa huduma za afya*
- *Wakazi wa vituo vya huduma za muda mrefu*
- *Wafanyakazi wa huduma za muda mrefu wanaotangamana na mgonjwa moja kwa moja*
- *Wafanyakazi na wajibu wa huduma za matibabu ya dharura*

Utambuaji wa Picha: CDC

Awamu Zijazo, tarehe hazijatangazwa:

- *Watu walio na hali za afya za hatari ya (zilizokadiriwa Machi baadaye)*

Machaguo ya kujisajili:

1. *Jisajili na Vermont Department of Health mtandaoni kwenye https://www.healthvermont.gov/covid-19/vaccine/getting-covid-19-vaccine (usajili wa mtandaoni kwa Kiingereza) au kwa kuwasiliana na simu ya dharura ya chanjo kwa 855-722-7878 (Kwa usaidizi katika lugha nyingine bonyeza 1). Saa za Kituo cha Usaidizi wa Simu ni Jumatatu-Ijumaa, saa 8:15 asubuhi – saa 5:30 alasiri na Jumamosi na Jumapili, saa 10:00 asubuhi – saa 3:00 alasiri.*

2. *Ikiwa una maswali ya ustahiki au unahitaji usaidizi wa usajili katika lugha nyingine, unaweza kuwasiliana na msimamizi wa kesi yako kwenye Association of Africans or the Refugee Program.*

Ikiwa huna msimamizi wa kesi, wasiliana na Refugee Program kwa 802-655-1963 au Association of Africans kwa 802-355-0795 na mtu atawasiliana nawe ambaye anazungumza lugha yako.

Emergency Rental Assistance Program (Mpango wa Usaidizi wa Upangaji wa Dharura)

Tarehe ya kuanza: *imekadiriwa katikati ya Machi 2021 (tarehe rasmi itaamuliwa)*

Anayestahiki:
Usaidizi huu wa fedha ni wa wale walioathiriwa vibaya na janga. Watumaji maombi watakuwa na mapato ya kutosha na matakwa mengine watakayohitaji kutimiza ili kustahiki.

Kile ambacho mpango unatoa:
Mpango unaweza kutoa usaidizi wa fedha ili kulipia kodi ya awali iliyochelewa na usaidizi wa upangaji wa baadaye. Ruzuku zitatolewa kwa nyongeza ya miezi mitatu na wapangaji wanaweza kutuma ombi la usaidizi kwa hadi miezi 12 kwa jumla. Huenda kukawa na chaguo la kutuma ombi la nyongeza ya miezi mitatu.

Mchakato:
Wamiliki wa majengo na wapangaji watahitaji kuwasilisha ombi na malipo yataenda moja kwa moja kwa mmiliki wa jengo. Kwa maswali au usaidizi wa kukamilisha ombi, wasiliana na Refugee Program kwa 802-655-1963 au Association of Africans Living in Vermont kwa 802-355-0795 na mtu atawasiliana nawe ambaye anazungumza lugha yako.

Ili kuona taarifa kuhusu mpango na ombi kwa Kiingereza, tembelea:
https://www.vsha.org/

Una Maswali? Unahitaji Usaidizi?

COVID-19 Resource and Recovery Center (RRC) ya Burlington ipo hapa kusaidia, wasiliana nasi kwa 802-755-7239 au recovery@burlingtonvt.gov na utume ujumbe ukiwa na jina lako, lugha unayopendelea na maelezo ya mawasiliano na tutakusaidia haraka iwezekanavyo. Kituo chetu cha usaidizi wa simu kina huduma za ukalimani wa simu. Saa zetu za kazi ni Jumatatu hadi Ijumaa, saa 8:00 asubuhi hadi saa 4:30 alasiri.

Pata Tafsiri:

Vermont Department of Health
https://www.healthvermont.gov/media/translation/covid-19-translations
City of Burlington
https://www.burlingtonvt.gov/covid-19/translated
Vermont Multilingual Task Force:
https://www.youtube.com/channel/UC3zjPpeFnXqvESr1y3d4DvQ

Taarifa zilizo katika waraka huu zinaweza kubadilika miongozo inaposasishwa kwenye ngazi ya taifa na jimbo

Utambuaji wa Picha: CDC na City of Burlington